

The Apostolic Life Community of Priests in the Opus Spiritus Sancti.



Africa Province.

E-Mail: alcp.africaprovince@yahoo.com

Office Mobile: +255 715 429 516

Provincialate Office
P. O. Box 734,
Moshi — Tanzania.

25th March, 2023

WARAKA-25th MARCH, 2023 KUPASHWA HABARI YA KUZALIWA BWANA

Wapendwa Mapadre, ALCP/OSS,

Salaam toka Makao ya Shirika-Kanda na Nyumba MAMA, Sabuko-Sanya Juu, Tanzania.

Ni muda tena tumepata wa pekee kufanya toba na malipizi kwa kipindi cha KWARESIMA kinachotuingiza kwenye maadhimisho ya PASAKA.

Leo tunaweka mbele yenu tafakari hii kuhusu **UTU WETU, UTU WA MWANADAMU**. “**Ut**u ni hadhi ya mwanadamu Utu wema ni hali ya kujali wengine na kuguswa na yale wanayoyapitia unaonekana katika kujali, kumuwazia mwingine mema, kuona hitaji la mtu na kumsaidia pasipo kuombwa au kuambiwa. Yesu Kristo ndiye kielelezo cha utu wema. Utu wema unatupelekea kuwa na uhai mpya rohani mwetu. Huu ni utu mpya unaoletwa na kutubu, kusamehe, sala hai, matendo ya huruma na maisha ya unyenyekevu. ... Huu unatuweka mbali na utu wa kale, utu wa giza na dhambi. Hivi, Kwaresima yetu tuombe tuwe imara katika utu kwani UTU ni sifa ya kitabia au kihulka ya hadhi ya mwanadamu. Sifa hii hujidhihirisha kwa njia ya moyo, akili na utashi. Kumbe kuwa imara katika utu ni kuwa na moyo imara, akili imara na utashi imara; yaani kutotetereka kwa kutokata tamaa. kutoyumbishwa na mawazo au mafundisho yasiyohusu Imani ya kweli na kutokuwa na msimamo (utashi wenye kigeugeu).” (Nukuu toka Waraka wa Kwaresima wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania).

SAFARI NJEMA YA KIROHO YA KWARESIMA NA MAADHIMISHO MEMA NA YA FURAHA YA PASAKA

1. Mwaka wa kwanza wa malezi, 2022/2023

Wapo vijana kumi na mbili (12) mwaka wa kwanza wa malezi, 2022/2023. Tunawaomba safari njema ya wito.

2. Mwaka wa pili wa malezi, 2022/2023

Wapo waseminari kumi na mbili (12) mwaka wa pili wa malezi, 2022/2023. Tunawaomba tafakari nzuri juu ya wito na maamuzi sahihi.